HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Simu: 026-2772614
Fax: 026-2772070
Email: ded@mufindi.go.tz
Web: www.mufindidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji

S.L.P. 223,

Mafinga.

Mh. Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
Hiki ni kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha kujadili taarifa mbalimbali za Fedha, Uongozi na Mipango. Kikao hiki kinafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa agizo namba 21.Kwa msingi huo ni jukumu la kila mjumbe kupitia taarifa hii na kuchangia maoni ambayo yataisaidia Halmashauri kufikia lengo kuu la kutoa Huduma nzuri na endelevu zenye kuleta Maendeleo katika Wilaya yetu ya Mufindi.

1) Mapitio ya Bajeti 2018/19

A) Mapato
Mh. Mwenyekiti,
Katika Mwaka wa Fedha wa 2018/19, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipitisha bajeti ya kukusanya na kupokea jumla ya **Tshs.56,359,048,777.00** Makusanyo haya yamegawanyika kama ifuatavyo;

Na.	Maelezo	Kiasi
1.	Mapato ya ndani	4,162,017,000.00
2.	Ruzuku Mishahara	35,229,626,720.00
3.	Ruzuku matumizi ya kawaida	1,312,132,000.00
4.	Ruzuku ya miradi ya maendeleo na Wadau wengineo	10,856,660,057.00
5	Nguvu za Wananchi	4,798,613,000.00
JUMLA		**56,359,048,777.00**

Aidha kwa mwaka wa fedha 2018/19, Halmashauri imeanza na bakaa ya**Tshs.1,164,911,096.50** Fedha hizi zimegawanyika kama ifuatavyo;

Jina la akaunti	Namba ya akaunti	Kiasi
Matumizi ya kawaida	9921210901	12,454,597.38
Miradi ya Maendeleo	9921210301	217,787,291.25

Maji	9921210701	38,715,509.76
Mapato ya ndani	60210001172	381,520,394.05
Akaunti ya Mishahara	9921210801	2,563,371.32
Elimu	9921210501	78,934,966.37
Afya	9921210601	432,934,966.37
Jumla		**1,164,911,096.50**

Mh. Mwenyekiti

Ukijumlisha fedha ya bakaa, makisio yaliyokuwa yameidhinishwa, bajeti ya Halmashauri kwa Mwaka 2018/2019 inakuwa na jumla ya **Tshs.57,523,959,873.50** kwa mchanganuo ufuatao;

Chanzo cha Mapato	**Kiasi**
Mapato ya ndani	4,608,093,466.37
Ruzuku ya Mishahara	35,229,626,720.00
Matumizi mengineyo	1,436,134,563.67
Nguvu za Wananchi	4,798,613,000.00
Miradi ya Maendeleo	11,451,492,123.46
Jumla	**57,523,959,873.50**

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Halmashauri ya wilaya ya Mufindi inategemea kutumia jumla ya **Tshs.57,523,959,873.50** Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo;

Chanzo cha Matumizi	**Kiasi**
Mishahara	35,229,626,720.00
Matumizi ya Kawaida	3,447,988,563.67
Miradi ya maendeleo	18,846,344,589.83
Jumla	**57,523,959,873.50**

Aidha katika kipindi cha Julai – Septemba 2018 jumla ya kiasi cha **Tshs 50,750,083,529.74** cha bajeti ya mwaka 2018/2019 pamoja na bakaa ndicho kilichoingizwa na Ofisi ya TAMISEMI katika mfumo wa Kielektroniki yaani Epicor kati ya jumla ya bajeti ya **Tshs 57,523,959,873.50** ya mwaka.Kumekuwa na changamoto za kimfumo ambapo bajeti za Halmashauri zinachelewa kuonekana kwenye mfumo wa Epicor, hata hivyo Halmashauri inaendelea kufanya jitihada za kufuatilia Ofisi ya

TAMISEMI ili kuhakikisha kuwa bajeti yote inaingizwa katika mfumo ili kuwa na mtiririko mzuri wa taarifa ya mapato na matumizi ya kila mwezi.

2) Hali Halisi

A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2018, Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya **Tshs.8,078,446,395.05** Kati ya Mapato haya **Tshs. 752,688,139.24** ni mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani, **Tshs.6,150,085,500** ni Mishahara, **Tshs.803,621,281.45** ni Miradi ya maendeleo na **Tshs.372,051,474.36** ni Matumizi ya kawaida.

Mlinganisho wa Mapato halisi ya **Tshs. 8,078,446,395.05** kwa kipindi cha Septemba 2018 na makisio yaliyoingizwa kwenye Mfumo ya **Tshs.49,585,172,433.24** ya mwaka 2018/19 unaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **16.29** ya lengo la mwaka wa fedha wa 2018/2019. Aidha mlinganisho wa mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Septemba 2018 ya **Tshs.752,688,139.24** na Makisio ya mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani ya **Tshs.4,162,017,000.00** kwa kipindi hicho, yanaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **18.08** ya lengo la mwaka .

Mh Mwenyekiti,

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha Julai 2018- Septemba 2018 unaonesha kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato haikuwa ya kuridhisha.

Hali hii inasababishwa na

- Kutokuwa na masoko ya kuuzia mbao kwa wafanyabiashara wanaochakata magogo eneo la Halmashauri ya Wilaya Mufindi
- Kuwa na msimu wa kiangazi katika mashamba ya chai hivyo kusababisha uzalishaji wa majani kupungua.
- Mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato wa GEPG kushindwa kutambua malipo yanayofanywa na makampuni ya chai yanayotumia benki ya CRDB,I&M na NBC
- Mwitikio mdogo wa wafanyabiashara kufanya uvunaji katika msitu wa SAO HILL kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji hivyo kutegemea misitu ya wavunaji katika misitu ya watu binafsi ambayo uzalishaji wake wa mbao ni mdogo
- Ukosefu wa magari ya kutosha kwa ajili ya kufanya doria na ufuatiliaji maeneo mbalimbali yanayokusanya mapato
- Kutokusanya leseni za biashara kama ilivyo kwenye bajeti kutokana na uhaba wa watumishi katika kitengo cha Biashara.
- Kuchelewa kuunganishwa na mfumo wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi unaowezesha kufanya miamala ya mauzo ya viwanja vilivyopo Mji mdogo wa Igowole

Ili kukabiliana na hali hii Halmashauri imejipanga kufanya yafuatayo

- Kuendelea kusimamia vyanzo vyote vya mapato hasa Kufanya doria kila mara ili kubaini wafanyabiashara wanaotorosha mazao ya misitu bila kulipia kwani ndicho chanzo kikubwa cha mapato .Aidha Halmashauri imeendelea kuimarisha kikosi kazi cha kukusanya mapato ili kufanya Doria hasa nyakati za usiku
- Kuomba kibali Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa cha kufungua akaunti katika benki ya CRDB,I&M na NBC ili Makampuni ya chai yaweze kulipa ushuru kwa wakati ambapo barua Kumb.Na.HW/MUF/F.20/8/VOL V/71 ya tarehe 11/9/2018 imeandikwa kupata kibali kutokana na miongozo ya Wizara ya Fedha
- Kuendelea kufanya ufuatiliaji wa kibali cha ununuzi wa gari jingine la mapato Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuboresha ukusanyaji mapato na kufuatilia kwa karibu matengenezo ya gari STJ 9910 la idara ya kilimo ambalo limepelekwa TEMESA ili kupunguza changamoto ya usafiri kwenye shughuli za mapato
- Kuanzisha/kutenga maeneo ambayo yatatumika kama sehemu ya kuuzia mazao ya misitu kama mbao katika maeneo yanayopatikana mazao haya kwa wingi ambapo kwa kuanzia imependekezwa kuanzisha soko la mbao Mtili katika eneo la Shamba la Halmashauri
- Kila idara kusimamia chanzo cha mapato ili kuhakikisha kinakusanywa kulingana na makisio iliyojiwekea.
- Kusimamia matumizi ya Mfumo wa Ki Electronic wa ukusanyaji wa mapato kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara.
- Kuongeza mashine (POS)za kukusanyia mapato katika maeneo ambayo bado hayajapatiwa mashine hizo ambapo katika robo ya pili zitaongezwa POS nyingine 10
- Kuendelea kuwatambua Wafanyabiashara wanaofanya biashara katika Eneo la mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Mufindi ili waweze kulipa kodi na Leseni za Biashara na kuendelea kutumia kikosi kazi cha kukusanya leseni za biashara ili kufikia malengo.
- Katika Mwaka wa fedha wa 2018/19, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kubadilisha utaratibu wa ukusanyaji wa ushuru wa magogo na mbao kwa kukusanya ushuru wa mbao kwa mbao zote zitakazochakatwa katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na kukusanya ushuru wa Magogo kwa wale wafanya biashara watakaosafirisha Magogo na Utaratibu huu kuanza Januari 2019
- Kuendelea na uhamasishaji kwa Wananchi kuhusu uuzwaji wa viwanja vya Igowole baada ya kukamilika uunganishwaji wa Mfumo wa kielektroniki wa Wizara ya Ardhi na kuwakumbusha watumishi waliokopeshwa viwanja kulipa kwa wakati uliokubalika
- Kuendelea kuhamasisha Jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti,

Matumizi hutegemea mapato yanayokusanywa. Kwa kipindi cha kuishia 30, Septemba 2018, Halmashauri imetumia kiasi cha T**shs.7,917,065,810.77** Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo,

Chanzo cha Matumizi	Kiasi
Mishahara	6,150,085,500.00
Matumizi Mengineyo	738,862,334.78
Miradi ya Maendeleo	1,028,117,975.99
Jumla	**7,917,065,810.77**

3) Taarifa Nyinginezo

a) Usuluhisho wa Benki

Mh. Mwenyekiti,

Usuluhisho wa benki kwa mwezi Septemba 2018 haujafanyika kwa akaunti mbili zilizobaki katika benki ya NMB Mafinga kutokana na kutotengemaa kwa mfumo na akaunti sita zilizofunguliwa na Benki kuu zinafanywa na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ufuatiliaji umefanyika Ofisi ya TAMISEMI na majibu yaliyotolewa ni kwamba mfumo uliotumika kuandaa bajeti ya 2018/2019 yaani PLANREP umekuwa na changamoto ya kuhamisha takwimu kwenda kwenye mfumo funganifu wa Malipo –EPICOR,hata hivyo jitihada zinaendelea katika ngazi ya Wizara ya TAMISEMI kufanya marekebisho ya kimfumo ili kurahisisha uandaaji wa taarifa mbalimbali za Halmashauri.

Na	Jina la Akaunti	Salio Benki NMB	Salio la Benki - NMB	Salio la Kwenye Vitabu
7	Deposit - 60210001177			
8	Own Source - 60210001172			

b) Akaunti ya Amana

Akaunti ya Amana huweka amana mbalimbali. Wakati tunaanza mwaka huu wa fedha (1/7/2018) mfuko huu ulianza na salio anzia la **Tshs.282,859,579.41** Mapato kwa mwezi Julai - Septemba 2018 yalikuwa **Tshs.66,512,681.14** na hivyo kuifanya Akaunti hii kuwa na jumla ya **Tshs.349,372,260.55** ilipofika tarehe 30/9/2018. Aidha Matumizi kwa Mwezi Julai – Septemba 2018 ni Kiasi cha **Tshs.49,885,000.00** na hivyo kufanya Akaunti hii kuwa na bakaa ya **Tshs.347,772,260.55**

c) Madeni

Mh. Mwenyekiti,

Halmashauri imefanya uhakiki wa madeni na kwamba kuanzia 1 Julai 2018 Halmashauri ilikuwa na deni la Tshs **311,190,046.70** ,ambapo hadi kufikia Agosti 2018 jumla ya deni la Tshs **35,451,995.50** lilikuwa limelipwa na kusalia kiasi cha Tshs **275,738,051.20**

Mh. Mwenyekiti,

Pamoja na Taarifa hii nimefungasha Jedwali Mbalimbali zinazoonesha mwenendo wa mapato na matumizi katika kipindi hiki, Madeni na malipo ya 25% kwa vijiji

Mh. Mwenyekiti,

Naomba Kuwasilisha.

Renatus J. Masonda
KNY: MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI